TAREHE 27 HADI 30 NOVEMBA 2023

LUSAKA, ZAMBIA

International CPHIA 2023 Conference on Public Health in Africa

# KONGAMANO LA 3 LA KIMATAIFA KUHUSU AFYA YA UMMA BARANI AFRIKA

## KUVUNJA MIPAKA: KUWEKA UPYA MSIMAMO WA BARA LA AFRIKA KWENYE MFUMO WA AFYA WA KIMATAIFA

### Muhtasari wa Uwasilishaji wa Muhtasari wa Utafiti wa Mkutano wa CPHIA 2023

### Kuhusu Mkutano wa CPHIA

Mkutano wa kila mwaka kuhusu Afya ya Umma Barani Afrika (CPHIA, Conference on Public Health in Africa) unatoa jukwaa la kipekee la kiafrika kwa viongozi katika bara nzima kutafakari kuhusu mafunzo yaliyopatikana katika sekta ya afya na sayansi, na kutafuta mwelekeo wa kukuza mifumo thabiti zaidi ya afya.

Mnamo Desemba 2022, wanasayansi, watunzi wa sera na mawakili 2,800 kutoka kote duniani walikutana ana kwa ana jijini Kigali, Rwanda, kwa ajili ya mkutano wa CPHIA 2022 ili kuangazia sayansi na ubunifu wa Kiafrika, na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, eneo na kimataifa, huku washiriki 11,625 wa ziada wakijiunga mtandaoni. Mkutano huu uliendeleza mafanikio ya mkutano wa kwanza kabisa wa CPHIA 2021, ulioangazia kuhusu jinsi ya kufanikisha maendeleo ya kudumu dhidi ya changamoto za muda mrefu na zinazoibuka za afya.

Kwa kupanua mipaka ya mkutano mara nyingine tena, mkutano wa CPHIA 2023 utaandaliwa jijini Lusaka, Zambia kuanzia tarehe 27 hadi 30 Novemba ili kuonyesha jinsi bara linavyovunja mipaka, kuthibitisha upya nafasi ya bara la Afrika kama kiongozi katika sekta ya sayansi na ubunifu, mzalishaji wa maarifa mapya na bidhaa za afya na kielelezo cha maendeleo. Nchi za kiafrika zinapoongeza kasi ya kufanikisha lengo la Mwelekeo Mpya wa Afya ya Umma (New Public Health Order), mkutano wa mwaka huu utasaidia kukuza bara la Afrika lenye afya na mafanikio zaidi – kwa ajili ya bara na ulimwengu.

### Mwaliko wa Kuwasilisha Mihtasari ya Utafiti

Waandalizi wa mkutano wa CPHIA 2023 wanafuraha kualika mihtasari ya utafiti ya mada zote za mkutano kutoka kwa mtu yeyote ambaye angependa kushiriki.

**Tarehe za Kuwasilisha Muhtasari wa Utafiti:** Waandishi wanapaswa kupakia mihtasari ya utafiti wao kupitia **mfumo wa mtandaoni wa kuwasilisha mihtasari ya utafiti wa Oxford.** Iwapo utatatizika kutumia mfumo huo, tafadhali wasiliana na **CPHIAabstracts@africa-union.org**.

- **Tarehe ya kuanza kuwasilisha:** Uwasilishaji wa mihtasari ya utafiti utaanza tarehe **21 Julai 2023**.
- **Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha:** Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha muhtasari wa utafiti ni

African Union | AFRICA CDC Centres for Disease Control and Prevention Safeguarding Africa's Health | Limeandaliwa na: Republic of Zambia | ZNPHI Zambia National Public Health Institute

tarehe **30 Agosti 2023 saa 23:59hrs CAT [21:59hrs UTC].** ***Hakuna mihtasari ya utafiti itakayokubalika baada ya tarehe rasmi ya mwisho.***

- **Utathmini**: Mihtasari yote ya utafiti iliyowasilishwa itakaguliwa na wakaguzi wasiopungua watatu.
- **Kukubaliwa**: Wawasilishaji wataarifiwa kuhusu kukubaliwa kwa mihtasari ya utafiti wao kufikia tarehe **30 Septemba 2023.**
- **Mkutano wa CPHIA:** Mihtasari ya utafiti iliyokubaliwa itawasilishwa katika mkutano wa CPHIA 2023 tarehe **27 hadi 30 Novemba.**

**Mada:** Mihtasari ya utafiti itakubaliwa kwa mada zifuatazo za mkutano:

- ***Mada ya 1:*** Utayari wa Kupambana na Mlipuko wa Janga na Mbinu Thabiti za Ufadhili za Afrika
- ***Mada ya 2:*** Kuhimiza Ubunifu wa Kiafrika: Kuimarisha Utengenezaji wa Ndani wa Chanjo, Vipimo na Matibabu
- ***Mada ya 3:*** Kutoa Bima ya Afya kwa Wote Barani Afrika: Mifumo ya Afya ya Usawa na Iliyoimarishwa
- ***Mada ya 4:*** Kwa Ajili ya Wanawake kutoka kwa Wanawake: Uwezo wa Kupata Huduma Bora za Afya kwa Wasichana Wadogo na Wanawake Barani Afrika
- ***Mada ya 5:*** Kulinda Usalama wa Sekta ya Afya Barani Afrika: Matukio ya Dharura ya Afya, Usalama wa Afya ya Watu, Mabadiliko ya hali ya anga na Mbinu za Ushughulikiaji za Sekta Nyingi
- ***Mada ya 6:*** Kubadilisha Sekta ya Afya Barani Afrika kupitia Ubunifu Dijitali
- ***Mada ya 7:*** Jamii Nzima: Nguvu za Kushirikisha Mashirika ya Kijamii, Sekta ya Kibinafsi na Wahisani wa Ndani
- ***Mada ya 8:*** Kupambana na Magonjwa ya Kuambukiza, NTD na Hali ya Virusi Kushinda Nguvu za Dawa Barani Afrika
- ***Mada ya 9:*** Kufichua Majanga ya Siri: Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza (NCD, Non-communicable Diseases), Afya ya Akili na Majeraha

**Ustahiki wa Mihtasari ya Utafiti na Waandishi:** Mihtasari ya utafiti halisi inayopatikana ndani ya mada za hapo juu ndiyo tu itakubaliwa kwa mkutano. Mwandishi mkuu lazima awe ameshiriki katika shughuli zinazoonyeshwa katika muhtasari wa utafiti na kupata idhini zinazohitajika za serikali wakati ambapo data nyeti inatumika katika muhtasari wa utafiti, pamoja na hati zozote muhimu za utiifu wa maadili.

Ingawa mtu anaweza kuwasilisha zaidi ya muhtasari mmoja wa utafiti, ni muhtasari mmoja pekee wa utafiti kwa kila mtu (mwandishi mkuu) utakaokubaliwa. Utafiti unapaswa kuwa umefanywa ndani ya kipindi cha mwaka wa 2020 hadi 2023 ili kuhakikisha ufaafu kwa mazingira ya sasa ya Kiafrika. Mihtasari ya utafiti ambayo imewasilishwa awali kwingineko itazingatiwa kwa hiari ya Kamati ya Muhtasari wa

Utafiti, lakini mihtasari ambayo bado haijawasilishwa katika mkutano mwingine wowote wa kisayansi ndiyo itakayozingatiwa zaidi. Waandishi wanapaswa kusisitiza jinsi kazi iliyofanywa ilivyotumika ili kuleta mabadiliko mazuri katika sekta ya afya na/au jinsi utafiti huo utakavyobadilisha mwelekeo wa sekta ya afya ya umma siku zijazo.

**Mgongano wa Maslahi:** Waandishi wa mihtasari ya utafiti iliyokubaliwa watapaswa kuwasilisha fomu ya ufumbuzi wa mgongano wa maslahi itakayoshirikiwa pamoja na barua ya kukubaliwa.

**Ufadhili wa Mihtasari ya Utafiti:** Huenda kukawa na idadi ndogo ya ufadhili unaopatikana ili kushughulikia gharama za usafiri na malazi kwa wawasilishaji wapya wa mihtasari ya utafiti. Iwapo ungependa kuomba ufadhili, utaulizwa wakati wa utaratibu wa uwasilishaji uweke alama ya tiki kwenye kisanduku ikiwa ungependa kuzingatiwa kwa msaada huu.

Kuomba msaada huu kutahitaji uwasilishe taarifa ya hitaji pamoja na muhtasari wa utafiti wako. Hata hivyo, tafadhali kumbuka kuwa hatua ya kuomba msaada huo *haimaanishi* umechaguliwa moja kwa moja kupokea ufadhili. Hakuna ufadhili utakaotolewa kwa wawasilishaji wa muhtasari wa utafiti ambao mihtasari ya utafiti wao haijachaguliwa kwa mawasilisho ya matamshi au mabango. Waombaji wataarifiwa ikiwa ufadhili wowote utatolewa pamoja na arifa ya kukubaliwa au kukataliwa kwa mihtasari ya utafiti wao.

## Muundo wa Muhtasari wa Utafiti

**Idadi ya maneno:** Muhtasari wa utafiti haupaswi kuzidi **maneno 300** (ambayo inajumuisha mada ndogo lakini haijumuishi mada kuu, maneno muhimu, orodha ya waandishi na anwani zao).

**Waandishi:** Waandishi wanapaswa kuorodheshwa kama ifuatavyo:

- **Mwandishi wa kwanza**: Andika jina la kwanza, herufi za kwanza za jina la kati (ikiwa lipo), na jina la mwisho (k.m., Henry M. Kuku).
- **Waandishi wenza:** Andika kila mwandishi mwenza kwa mpangilio wa mchango wao kwa kuandika majina yao ya kwanza na herufi za kwanza za jina la mwisho, kisha jina kamili la mwisho (k.m, J.N. Toto, C.H. Kwakweri).
- Andika mashirika yanayohusishwa na mwandishi wa kwanza na waandishi wote wenza.
- Onyesha mwandishi husika kwa Kinyota* na uandike anwani yake ya barua pepe na nambari ya simu pamoja maelezo yake mengine ya mawasiliano.

**Maneno muhimu**: Tafadhali jumuisha maneno muhimu 4 hadi 6

# KONGAMANO LA 3 LA KIMATAIFA KUHUSU AFYA YA UMMA BARANI AFRIKA

## KUVUNJA MIPAKA: KUWEKA UPYA MSIMAMO WA BARA LA AFRIKA KWENYE MFUMO WA AFYA WA KIMATAIFA

**Kichwa:** Kichwa kinapaswa kuwa cha kimaelezo lakini kifupi bila vichwa vidogo au vifupisho/akronimi na kinapaswa kuangazia hoja ya utafiti/mada hii inamaanisha ***nini***, ***mahali*** ulipofanyika na ***wakati*** ulipofanywa (k.m., Kundi la visa vya ugonjwa wa COVID-19 katika wilaya ya Keke, Agosti 2020). Andika kichwa kwa muundo wa sentensi na uandike tu majina ya watu/vitu na majina ya kisayansi kwa herufi kubwa panapofaa (k.m., Plasmodium *falciparum)*.

**Utangulizi/Maelezo Ya Msingi:** Toa maelezo ya msingi ya kisayansi, sababu ya utafiti, pamoja na umuhimu wa utafiti kwa afya ya umma. Kwa sababu ya utofauti unaotarajiwa wa wakaguzi na wanaohudhuria mkutano, usichukulie kwamba kila mtu atakuwa na ufahamu wa mada yako. Eleza kwa nini utafiti wako ni muhimu na swali/maswali yatakayojibiwa na utafiti huo. Maelezo ya msingi yaliyotolewa vizuri huweka msingi na yanapaswa kujumuisha:

- Maelezo mafupi ya mada na umuhimu wake kwa afya ya umma
- Malengo ya utafiti
- Maswali ya utafiti au nadharia ya utafiti ikiwa inahitajika

**Mbinu:** Eleza mbinu zilizotumiwa kwa utafiti. Hoja muhimu za kujumuishwa ni:

- Muundo wa utafiti
- Mazingira ya utafiti
- Kundi la utafiti
- Vigezo vya ustahiki na ufafanuzi wa tukio, ikiwa lipo
- Ukubwa wa sampuli na mbinu za kukusanya sampuli
- Udhibiti na uchanganuzi wa data

**Matokeo:** Wasilisha matokeo muhimu (mazuri na mabaya) ya utafiti yanayohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Sehemu hii **haipaswi** kujumuisha majadiliano ya matokeo. Toa nambari kamili na asilimia/viwango, kiasi na uwiano wake panapohitajika. Tafadhali kumbuka kwamba kwa sababu muhtasari wa utafiti ni hati ya kujitegemea na inayoweza kurejelewa, sehemu ya matokeo inapaswa kuwa na data.

Haipaswi kujumuisha kauli kama vile “Data itajadiliwa.” Ikiwa bado kazi kubwa haijakamilika kabla ya kuwasilisha muhtasari wa utafiti wa mkutano, tafadhali onyesha kwamba matokeo hayo si rasmi.

**Hitimisho:** Fupisha kadri uwezavyo. Usieleze upya data iliyojumuishwa katika matokeo. Sehemu hii inaweza kujumuisha:

- Ufafanuzi wa matokeo muhimu na athari yake kwa sekta ya afya ya umma
- Hatua za afya ya umma zinazopendekezwa na/au zilizotekelezwa kama matokeo ya utafiti

TAREHE 27 HADI 30 NOVEMBA 2023

LUSAKA, ZAMBIA

International CPHIA 2023 Conference on Public Health in Africa

# KONGAMANO LA 3 LA KIMATAIFA KUHUSU AFYA YA UMMA BARANI AFRIKA

## KUVUNJA MIPAKA: KUWEKA UPYA MSIMAMO WA BARA LA AFRIKA KWENYE MFUMO WA AFYA WA KIMATAIFA

***Kumbuka:*** Huwezi kufanya mabadiliko kwenye muhtasari wa mwisho wa utafiti baada ya kuwasilishwa. Hata hivyo, iwapo muhtasari wa utafiti wako utachaguliwa kwa wasilisho na umefanyiwa mabadiliko makubwa baada ya kukubaliwa, mabadiliko hayo yanapaswa kuangaziwa kwenye bango au wasilisho la muhtasari wa utafiti.

### Vigezo vya Utathmini

Kila muhtasari wa utafiti utatathminiwa na wakaguzi watatu huru kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- Maelezo ya msingi na sababu ya utafiti
- Ufaafu wa mbinu
- Uwasilishaji wa matokeo
- Hitimisho na ufafanuzi wa matokeo
- Umuhimu kwa afya ya umma
- Uelewekaji wa jumla wa muhtasari wa utafiti
- Uhalisi wa utafiti
- Ufaafu kwa mada/dhamira ya mkutano

### Maamuzi na Hatua Zinazofuata

**Uchapishaji katika Jarida kuhusu Afya ya Umma Barani Afrika:** Mihtasari yote ya utafiti iliyokubaliwa itachapishwa katika Jarida kuhusu Afya ya Umma Barani Afrika la CDC ya Afrika katika Kitabu rasmi cha Mihtasari ya Utafiti cha mkutano wa CPHIA 2023.

**Mawasilisho ya Moja kwa Moja na Ukumbi wa Mabango:** CPHIA 2023 ni mkutano wa kudhudhuria ana kwa ana. Wawasilishaji wote wa mihtasari ya utafiti, iwe imechaguliwa kwa wasilisho la matamshi au mabango, wanatarajiwa kuweza kuhudhuria mkutano huo jijini Lusaka, Zambia, ikiwa watachaguliwa.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu mkutano wa CPHIA 2023, tembelea [www.cphia2023.com](http://www.cphia2023.com) au tuma barua pepe kwa Katibu wa mkutano wa CPHIA kupitia [CPHIAsecretariat@africa-union.org](mailto:CPHIAsecretariat@africa-union.org).**

**Kwa maswali kuhusu mpango wa mihtasari ya utafiti, tafadhali tuma barua pepe kwa [CPHIAabstracts@africa-union.org](mailto:CPHIAabstracts@africa-union.org).**

[MWISHO]